Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEKIMA NI UHURU

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

Toleo la 04

# Jarida la HEET UDSM

**Toleo la Disemba 2023-Machi 2024**

# HEET

Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi







Katika toleo hili...


**Mapitio ya Mitaala** *Kuendana na Vipaumbele vya Taifa* — **Uk 5**

**Mpango Endelevu wa** *Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa HEET uko Mbioni Kuandaliwa* — **Uk 9**

**UDSM Waandaa Mwongozo** *wa Uambatishaji wa Wafanyakazi* — **Uk 15**

**Kamati ya Bajeti ya Baraza** *la Wawakilishi Zanzibar Yatembelea UDSM* — **Uk 18**

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| *Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo* | **3** |
| *Ujumbe wa Mratibu* | **4** |
| *Mapitio ya Mitaala Kuendana na Vipaumbele vya Taifa* | **5** |
| *Mradi wa HEET Wang'ara katika Mahafali ya UDSM 2023* | **6** |
| *Prof. Killian Awataka Viongozi Wanawake UDSM Kuzingatia Dhana ya Mageuzi katika Uongozi* | **8** |
| *Mpango Endelevu wa Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa HEET uko Mbioni Kuandaliwa* | **9** |
| *Ujumbe wa Naibu Mratibu* | **10** |
| *Tahariri* | **11** |
| *Matukio katika Picha* | **12** |
| *Mfumo wa Ubunifu wa Usimamizi wa Mradi Kuongeza Ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi* | **14** |
| *UDSM Waandaa Mwongozo wa Uambatishaji wa Wafanyakazi* | **15** |
| *Taasisi za Elimu ya Juu zatakiwa kuimarisha Mkakati wa Udhibiti wa Vihatarishi katika Mradi wa HEET* | **16** |
| *Shairi: "Nyota yang'ara Mlimani"* | **17** |
| *Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar Yatembelea UDSM-HEET* | **18** |

# Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo



Prof. William A. L. Anangisye

**Makamu Mkuu wa Chuo**

Ninawakaribisha wasomaji wetu wote katika Jarida la HEET- UDSM, toleo la Disemba 2023. Toleo hili linatoka wakati tukiwa katika shamrashamra za sikukuu za mwisho wa mwaka ambapo kila mmoja wetu anasherehekea mafanikio aliyoyapata kwa kipindi cha miezi 12. Vilevile Chuo kinalichukulia toleo hili kama jukwaa la kutoa salamu za mwisho wa mwaka kwa wadau wote wa Mradi wa HEET-UDSM, na Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ujumla wake.

Tukiwa tunasherehekea sikukuu hizi, tunalenga kufikia lengo endelevu la Mradi wa HEET. Kwa maana hiyo, utekelezaji wa Mradi wa HEET utaendelea kujikita katika mihimili mitatu ya Dira ya UDSM ya 2061, ambayo ni ari kwa wafanyakazi na wanafunzi; uongozi wenye maono; na rasilimali endelevu.

Aidha, Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kinapaswa kuzingatia kwamba tunaelekea katika mapitio ya kati ya Mradi ambayo yanatarajiwa kufanyika mwezi Mei, 2024. Tukiwa tunakaribia muda wa kufanya mapitio, Chuo kinafanya tathmini kuhusu mchango wa Mradi wa HEET katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Chuo 2020/2021-2024/2025.

Vitengo vya Kitaaluma vinapaswa kufanya tathmini juu ya mambo yaliyotekelezwa na yale yaliyoshindikana katika mchakato wa mapitio ya mitaala ili kuendana na matakwa ya tathmini ya kati ya Mradi. Msisitizo mkubwa unapaswa kuelekezwa katika mahitaji ya msingi yanayohitajika katika utekelezaji wa mitaala iliyopitiwa. Ni kupitia mahitaji hayo, ndipo Chuo kitafanya jitihada ya kuweka mkakati wa kupata rasilimali zinazohitajika kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Mchakato wa kubaini mahitaji ya msingi yanayohitajika unapaswa kufanyika bila kuathiri kasi ya utekelezaji wa Mradi. Menejimenti inafanya jitihada kuhakikisha kwamba angalau 45% ya bajeti ya Mradi kuwa imetekelezwa wakati wa kufanya tathmini ya kati ya Mradi. Kwa hiyo, msisitizo wetu katika kuanza shughuli za ujenzi kwenye maeneo yote ya Mradi ni muhimu sana. Ukamilishaji wa mapitio ya mitaala, utekelezaji wa shughuli za kuwa na kampasi maizi na kumaliza kwa wakati kwa wanafunzi walionufaika na ufadhili wa Mradi wa HEET pia ni maeneo yanayopewa kipaumbele cha hali ya juu.

Utekelezaji wa Mradi wa HEET umefanikiwa kutokana na ufadhili kutoka kwa wadau mbalimbali. Menejimenti pia inatoa shukrani kwa Serikali, Benki ya Dunia, Jumuiya ya Chuo Kikuu na wanahabari. Tunajisikia fahari kuwa na wabia wetu katika utekelezaji wa Mradi wa HEET kwani mafanikio yetu mbali na mambo mengine yametokana na mambo mengi tuliyojifunza kutoka kwao. Chuo kinaahidi kuendelea kufungua milango kwa kuweka mazingira rafiki ya fursa ya kubadilishana uzoefu kutoka kwa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa Mradi.

Tukiwa tunasherehekea sikukuu hizi za mwisho wa mwaka, ninatumia wasaa huu kuwashukuru nyote na kuwatakia Heri ya Krismasi na Mwaka mpya wa 2024. Karibuni sana tusome Jarida hili.

# Ujumbe wa Mratibu



## Prof. Bernadeta Killian

### Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

Ninafurahi kuwajuza wadau wetu wa Mradi wa HEET kuhusu maendeleo yaliyopatikana tangu toleo la mwisho la Jarida letu lilipotoka. Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kimeendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mradi kulingana na Mpango wa Uwekezaji wa Chuo Kikuu ulioidhinishwa.

Kwa upande wa maendeleo ya miundombinu, hatua kadhaa zimefikiwa tangu kutolewa kwa toleo lililopita. Washauri wa kitaalamu wameendelea na mapitio ya usanifu wa kazi za ujenzi zilizopangwa kufanyika Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi. Zabuni kwa wakandarasi wa ujenzi wa majengo yanayotarajiwa kujengwa Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi ilitangazwa, kufunguliwa na sasa iko katika hatua ya mwisho ya tathmini kabla ya mikataba kusainiwa.

Baadhi ya hatua zinazohusisha shughuli za ujenzi zimefikiwa katika kampasi ya Kagera. Zabuni kwa ajili ya washauri wa kitaalamu katika shughuli za usanifu, mapitio na usimamizi zimetangazwa, mchakato wa kupata orodha ya washauri wa kitaalamu umefanyika na hivi sasa uko katika hatua za mwisho za tathmini ya mapendekezo na kusainiwa kwa mkataba. Wakati huohuo, zabuni kwa ajili ya wakandarasi wa ujenzi wa majengo katika maeneo ya Kampasi ya Kagera imetangazwa.

Kwa upande wa uboreshaji wa mitaala na zana za kufunzia na kujifunzia, vitengo vya kitaaluma viko katika mchakato wa mapitio baada ya kupitia katika hatua mbalimbali. Mathalani, vitengo vimefanya utafiti fuatilizi na mkutano na wadau. Aidha, Chuo kimeanzisha mchakato wa kupata miongozo ya ufundishaji wa kiubunifu ili kuwa na mitaala bora. Miongozo hiyo iko katika hatua ya mapitio na kupata maoni ya wadau wa ndani kabla ya hatua ya kuidhinishwa.

Baadhi ya hatua za kujenga na kuimarisha uhusiano baina ya Chuo na sekta ya ajira zimefikiwa ambapo wafanyakazi waliokwenda kufanya kazi katika tasnia mbalimbali kwa mkataba maalum wamekamilisha kazi zao kwa ufanisi. Wanataaluma watano waliopata ufadhili wa masomo yao ya umahiri kupitia Mradi wa HEET wamehitimu mafunzo yao katika taaluma za sayansi kutoka katika vyuo mbalimbali nchini Uingereza na wamekwisharipoti katika kituo chao cha kazi. Usambazaji wa mifumo ya TEHAMA na mitandao ya msingi unaendelea na kwa kiasi kikubwa shughuli za usimikaji wa mfumo zitafanyika Januari 2024.

Kwa upande wa shughuli mtambuka, tumefanikiwa kuwasilisha taarifa za ESIA kwa maeneo yote kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya mapitio na mapendekezo kwa Benki ya Dunia kwa lengo la kuidhinishwa. Timu inayosimamia masuala ya usalama inaendelea na awamu ya pili ya ushirikishwaji wa wadau. Mikutano kadhaa ambayo imeishirikisha Ofisi ya rasilimaliwatu, wafanyakazi waendeshaji, wafanyakazi wa Kurugenzi ya Miliki, Polisi Wasidizi, UDASA na DARUSO imefanyika.

Kwa upande mwingine timu ya mradi imewashirikisha viongozi wa Mkoa wa Kagera kwa kuwapa ufafanuzi kuhusu hali ya maendeleo ya ujenzi katika Kampasi ya Kagera. Tumefurahi kusikia kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Fatma Mwasa, akiahidi kutoa ushirikiano wa dhati katika ujenzi wa Kampasi ya Kagera.

Aidha, Mradi ulifanikisha mafunzo ya siku moja kwa viongozi wanawake kutoka UDSM yaliyofanyika mwezi Disemba 2023 ambapo viongozi hao walipata mafunzo ya masuala yanayohusiana na usawa wa kijinsia, mageuzi ya kiuongozi, usimamizi wa fedha na masuala yanayoibua hisia kwa watumishi.

Katika kipindi hiki wajumbe wa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi walipatiwa mafunzo ya aina mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo katika utekelezaji na usimamizi wa Mradi. Mathalani, wajumbe walishiriki mafunzo ya siku tano kuhusiana na udhibiti wa vihatarishi. Kwa kuzingatia mafunzo hayo, washiriki hao wanatarajiwa kutumia maarifa waliyoyapata kuandaa mfumo wa udhibiti wa vihatarishi na usajili wa vihatarishi hivyo. Chuo kiko katika mchakato wa kumteua mratibu wa udhibiti wa vihatarishi katika Mradi wa HEET.

Chuo daima kimekuwa kitovu cha mafunzo kwa wadau wetu kutoka maeneo mbalimbali. Katika kutekeleza dhamira hii, katika kipindi hiki, tunajivunia kuvipokea vikundi vingi vya watu kutoka taasisi kadhaa waliokitembelea Chuo kwa lengo la kujifunza kutokana na uzoefu wetu katika utekelezaji wa Mradi wa HEET. Mathalani, tulipokea wajumbe kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Kamati ya Bajeti kutoka Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka Zanzibar.

Tunapoelekea kuumaliza mwaka wa 2023 na kuukaribisha mwaka wa 2024, Chuo kinawatakia wadau wetu wote sikukuu njema ya Krismasi na heri ya mwaka mpya wa 2024 na sina shaka mtafurahia kwa mara nyingine kusoma Jarida letu la UDSM kuhusiana na Mradi wa HEET.

# Mapitio ya Mitaala Kuendana na Vipaumbele vya Taifa

*Na Zamda George, UDSM-HEET*





*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa (picha ya kulia) akizungumza wakati wa kikao cha Marasi, Maamidi na Wakurugenzi (picha ya kushoto) kujadili maendeleo ya mchakato wa mapitio ya mtaala Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kikao kilifanyika Chuoni mwezi Novemba, 2023. Kulia kwake ni Prof. Masoud Muruke, Mratibu, Mradi wa HEET katika upande wa mchakato huo wa mapitio ya mtaala.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimevunja rekodi ya maendeleo makubwa katika mchakato wa mapitio ya mitaala, unaoendelea huku ukienda sambamba na Dira ya UDSM ya 2061. Aidha, Chuo kimejiwekea mkakati wa kukamilisha mchakato huo kwa muda uliopangwa.

Akizungumza katika Mkutano wa Marasi, Maamidi na Wakurugenzi kutoka katika vitengo mbalimbali vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusiana na maendeleo ya mchakato wa mapitio uliofanyika katikati ya mwezi Novemba, 2023, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa alisema mchakato umepiga hatua kubwa na unatarajiwa kuzingatia mahitaji mbalimbali ya wadau.

Prof. Rutinwa amesema mchakato huo umepiga hatua kubwa huku ukiwianisha mahitaji ya kitaaluma, wadau na maendeleo ya taifa.

"Mchakato wa mapitio ya mtaala ni hatua muhimu katika kutafsiri Mpango Mkakati wa Chuo kwa vitendo na kuuoanisha na Dira ya UDSM ya 2061. Lengo kuu la mpango huu wa mapitio ya kina ya mtaala wa Chuo Kikuu ni kuhakikisha mitaala inakidhi matakwa ya jamii kwa maendeleo ya taifa", amesema Prof. Rutinwa.

Prof. Rutinwa ameendelea kueleza kwamba mchakato wa mapitio ya mitaala ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba elimu tunayotoa siyo tu inaendana na mahitaji ya jamii bali pia inaweza kubadilika ili kukidhi matakwa ya soko la ajira.

Mkutano huu ulihudhuriwa na viongozi kutoka vyuo vishiriki viwili, ndaki saba, shule kuu saba, na taasisi saba pamoja na waratibu mapitio ya mitaala kutoka katika vitengo vyote vya kitaaluma.

Aidha, washiriki kutoka maeneo mtambuka ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Jinsia na Kitengo cha Watu wenye Mahitaji Maalum, Kurugenzi ya Umataifishaji, Jumuiya ya Wahitimu na Uendelezi Chuo, na Kituo cha Mabadiliko ya Tabianchi walihudhuria mkutano huo. Mkutano huo pia ulihusisha mjadala kuhusu kozi zenye mlengo wa ubunifu, kozi za kusomwa mkondoni na zile za ana kwa ana na mkondoni kwa mitaala inayofanyiwa mapitio.

Msingi mkuu wa mkutano huo ulikuwa kutathmini maendeleo ya kila kitengo cha kitaaluma katika mchakato wa mapitio ya mitaala. Kimsingi, vitengo vyote vilishiriki katika utafiti fuatilizi, uchambuzi uliojikita katika maeneo manne ambayo ni umadhubuti, udhaifu, fursa na matishio.

Aidha, vitengo hivyo vimezingatia maoni ya wadau ambayo matokeo yake kwa ujumla ni kuunganishwa, kufutwa na kuundwa kwa kozi mpya. Mchakato huu ni ishara madhubuti katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Aidha, maeneo muhimu matano yalizingatiwa yakijikita katika maudhui na mbinu ya ufundishaji. Maeneo hayo ni maudhui (kuhakikisha mtaala unatoa maarifa muhimu na yanayohitajika); kujenga ujuzi (kutathmini kama mtaala unakuza uwezo wa kiutendaji); mbinu za kufundisha (kuchunguza ujuzi unaopatikana katika ufundishaji wa ubunifu); teknolojia ya kufundishia (kuimarisha matumizi teknolojia katika ufundishaji; na kushughulikia masuala mtambuka (kuzingatia masuala ya jinsia, na makundi ya watu wenye mahitaji maalum, umataifishaji, mabadiliko ya tabianchi).

Vitengo vyote vya kitaaluma vimetakiwa kukamilisha mchakato wa mapitio ifikapo Disemba 31 2023 kwa kuzingatia kalenda ya taifa. Baada ya mawasilisho ya kina kutoka katika vitengo vya kitaaluma yaliyoainisha mafanikio, changamoto na namna ya kukabiliana nazo, Prof. Rutinwa pia aliwakaribisha wataalamu wa nyanja mtambuka ambao walionekana kuwa na mchango mkubwa katika mchakato huu ili kutoa maoni yao.

### *Mawazo ya wataalam*

Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia na Mtaalamu wa Masuala ya Jinsia na Elimu Jumuishi katika Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Lulu Mahai alisisitiza umuhimu wa kuwa na kozi zinazozingatia masuala ya jinsia na kuvitaka vitengo kushirikiana na ofisi yake katika suala hilo kila itakapobidi.

Dkt. Edmund Mabhuye, Mratibu wa Kituo cha Taaluma ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mtaalamu wa Mazingira katika Mradi wa HEET-UDSM alisisitiza umuhimu wa kuzingatia suala la mazingira katika mapitio ya mtaala. Aidha, alitambua mafanikio yaliyopatikana katika miradi inayohusiana na mazingira inayoendeshwa na Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT) na Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET).

Dkt. Augustina Alexander, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Umataifishaji, Jumuiya ya Wahitimu na Uendelezi Chuo alihimiza mtazamo wa kimataifa wenye upekee katika masuala ya Kiafrika. Dkt. Sarah Kisanga, Meneja wa Kituo cha Huduma za Watu wenye Mahitaji Maalum, aliangazia nguzo nne za ujumuishi ambazo ni: upatikanaji wa maudhui, upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia, shughuli jumuishi za ujifunzaji, na modeli jumuishi ya tathmini.

Dkt. Ellen Kalinga kutoka Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano alitoa maoni ya msingi kwa mitaala kuzingatia masuala mtambuka ya teknolojia na kuhimiza umuhimu wa teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji.




*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (katikati-waliokaa) na viongozi wengine wa Chuo wakiwa na wahitimu wa kike wa shahada ya Uzamivu katika Mahafali ya 53 ya UDSM yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi Novemba, 2023.*

# Mradi wa HEET Wang'ara katika Mahafali ya UDSM 2023

Na Jackson Isdory, UDSM-HEET

Katika kusherehekea mafanikio ya kitaaluma, mahafali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yaliyofanyika Oktoba na Novemba, 2023 mbali na mambo mengine, yamebainisha mafanikio yaliyopatikana kutokana na Mradi wa HEET.

Katika mahafali hayo, takwimu muhimu zilibainishwa zikiangazia mafanikio ya Mradi wa HEET. Uwekezaji mkubwa wa kifedha umefanyika kupitia Mradi huu ambapo dhamira ya dhati ya kufanikisha malengo ya Mradi imedhihirika.

Makamu Mkuu wa Chuo aliweka bayana kuhusu muda wa Mradi na malengo ya muda mrefu ya kuboresha mfumo wa elimu kupitia Mradi huu.

Miongoni mwa maeneo muhimu yanayoangaziwa katika Mradi huu kufuatia mapitio ya mitaala ni kuwianisha mafunzo yanayotolewa katika programu zetu na mahitaji halisi ya soko la ajira.

Akitoa maelezo kuhusu Mradi huu, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa amesema "Mchakato wa mapitio ya mitaala umekwenda mbele zaidi ya programu za kipaumbele na badala yake programu zote zimepitiwa ili kuhakikisha kwamba wahitimu siyo tu wanatunikwa digrii zao, bali pia wanapata ujuzi utakaowawezesha kukabiliana na changamoto katika uchumi wa dunia."

Dhamira ya Mradi wa HEET katika kufanya mageuzi kwenye mazingira ya kufundishia na kujifunzia inajidhihirisha katika jitihada za kuboresha miundombinu, mfumo wa teknolojia na uwezeshaji wa wanataaluma.

Kwa upande mwingine, jitihada za kuimarisha usimamizi katika taasisi za elimu ya juu zilidhihirishwa katika mahafali hayo. Mageuzi katika mifumo ya serikali, uimarishaji wa utawala, na mipango ya kujenga uwezo kwa ujumla vimeinua kiwango cha usimamizi wa taasisi, na kuweka msingi wa kuwa na elimu bora yenye manufaa kwa jamii.

Mradi wa HEET unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umeonekana kuwa kinara katika mabadiliko chanya, ambayo yamelenga kuboresha mazingira ya kujifunzia, kuwianisha programu za kipaumbele na mahitaji halisi ya soko la ajira, na kuimarisha usimamizi wa jumla wa taasisi za elimu ya juu nchini Tanzania.

"Mradi wa HEET, ambao ni matunda ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Benki ya Dunia, umekuwa chachu ya mageuzi katika elimu nchini Tanzania. Kwa kuzingatia dhamira ya kuboresha mazingira ya kujifunzia, kuwianisha mafunzo yanayotolewa katika programu mbalimbali na soko la ajira, na kuimarisha usimamizi wa taasisi za elimu ya juu, Mradi umedhamiria kuleta mabadiliko chanya kwa mustakabali wa taifa letu", amesema Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa HEET-UDSM.



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete (katikati) akizungumza na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar (wa kwanza kulia), Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye (wa pili kulia), Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa (wa kwanza kushoto) na aliyewahi kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utawala, Prof. Yunus Mgaya (wa pili kushoto) muda mfupi kabla ya maandamano ya kitaaluma katika Mahafali ya 53 ya UDSM yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi Novemba, 2023.*

## Mafanikio kwa upande wa wanafunzi

Mafanikio makubwa kwa wanafunzi ambao ni wanufaika wa msingi wa Mradi wa HEET yamedhihirika katika mahafali hayo. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa na idadi ya wahitimu pamoja na kuridhika kwao kuhusu mwenendo wa Mradi huu ni sehemu ya manufaa ya Mradi.

Akizungumza baada ya mahafali Bw. Spencer Minja, mhitimu wa Shahada ya Awali ya Elimujamii katika Saikolojia alisema "Nimesikia kuhusu Mradi wa HEET na malengo yake hususani katika kipengele cha mapitio ya mitaala na uboreshaji wa mazingira ya kufunzia na kujifunzia. Ni matumaini yangu kwamba jitihada hizi zitazaa matunda na hatimaye wanaosoma programu hizo watahitimu wakiwa na ujuzi na maarifa yanayohitajika katika taaluma walizosomea".

## Kujenga mshikamano na Kuanzishwa kwa Ofisi ya Ushirikiano

Katika kujenga ari ya ushirikiano katika Mradi, suala la ushirikiano na asasi za serikali na zisizo za serikali limekuwa likisisitizwa sana. Kama ilivyosisitizwa katika mahafali haya, kuna umuhimu wa elimu inayotolewa kuwiana na mahitaji halisi yaliyoko katika jamii. Katika kutekeleza azma hii, kumeanzishwa ofisi ya Ushirikiano baina ya Chuo na Tasnia ya ajira.

Mkuu wa Ushirikiano baina ya Chuo na Tasnia Dkt. Eva Shayo akizungumzia kuhusu ofisi yake amesema "Ubia baina ya wadau unahusisha ushirikiano baina ya UDSM na wadau wengine mbalimbali ambao ni pamoja na taasisi za serikali, sekta binafsi, taasisi zisizo za serikali, mawakala wa serikali, asasi za kimataifa na wabia wa maendeleo. Umuhimu wa ushirikiano huu ni kuhakikisha kwamba Chuo kinatoa huduma inayohitajika katika soko la ajira.

## Mipango ya baadaye

Baada ya kubainisha mafanikio makubwa kama yalivyoainishwa katika mahafali haya, jitihada zaidi zimewekwa katika mafanikio ya baadaye. Matarajio ni kuwa na mafanikio endelevu yanayolenga kuboresha mfumo wa elimu ya juu nchini Tanzania. Kuhusiana na suala hili, Mratibu wa HEET UDSM, Prof. Bernadetha Killian, anasisitiza kwamba "UDSM kitahakikisha kwamba malengo yote ya mradi yanafikiwa kwa kiwango na ubora unaotakiwa"

Mafanikio ya Mradi wa HEET yaliyoainishwa katika sherehe za mahafali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni uthibitisho wa uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya elimu ya juu, na kujenga mazingira ya kitaaluma yanayoendana na mahitaji ya jamii kwa wakati husika. Jambo muhimu la kuzingatia hapa ni kwamba mafanikio haya hayaishii tu kusherehekea mafanikio ya kitaaluma bali pia ni uthibitisho thabiti wa mustakabali bora wa elimu ya Tanzania.



*Baadhi ya wahitimu katika Mahafali ya 53 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiwa na furaha kubwa wakati wa maandamano ya kitaaluma ya mahafali hayo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, mwezi Novemba, 2023.*



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaama Prof. Bernadeta Killian (Kushoto) akizungumza katika warsha ya viongozi wanawake wa UDSM na wale waliopandishwa ngazi za kitaaluma hivi karibuni (picha ya katikati na ya kulia). Warsha hiyo ilifanyika mwezi Disemba 2023 katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere, Mjini Kibaha, Mkoa wa Pwani.*

# Prof. Killian Awataka Viongozi Wanawake UDSM Kuzingatia Dhana ya Mageuzi katika Uongozi

*Na Zamda George, HEET-UDSM*

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala Prof. Bernadeta Killian amewataka viongozi wanawake kutoka UDSM kuzingatia uongozi wa mageuzi ambao utasaidia katika kujenga utamaduni wa usawa na jumuishi.

Prof. Killian ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM, ameyasema hayo katika warsha ya viongozi wanawake na wale ambao wamepandishwa ngazi za kitaaluma hivi karibuni. Warsha hii ilifanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere kilichopo Kibaha katika Mkoa wa Pwani.

"Uongozi wenye ufanisi huwa ni zaidi ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku; unahusisha utekelezaji wa malengo na kujenga ushirikiano, hasa kwa kuzingatia changamoto mahususi zilizopo na fursa za kipekee walizonazo viongozi wanawake katika kukabiliana na hali hii", amesema Prof. Killian.

Prof. Killian aliwaongoza washiriki katika mjadala wa kina juu ya Mageuzi ya kiuongozi kwa mtazamo wa kijinsia, akisisitiza jukumu muhimu la uongozi wa mageuzi. Warsha hiyo, iliyofadhiliwa na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), ilikusudiwa kuongeza uwezo wa uongozi wa mageuzi kwa viongozi wanawake, kwa kuzingatia uwezeshaji wa wanawake katika masuala ya kitaaluma na kifedha.

Katika semina hiyo pia, washiriki walipata fursa ya kujifunza namna ambavyo wanawake wanaweza kuimarisha utendaji wao unaozingatia weledi katika ulimwengu shirikishi ambapo walipata madondoo mbalimbali kutoka kwa Bi. Miranda Naiman, Mwasisi na Msimamizi Mkuu wa Empower Limited.

Bi. Naiman alitoa uzoefu wake katika suala la Uongozi wa mwanamke katika ulimwengu shirikishi ambapo msisitizo unawekwa katika utambuzi wa malengo na thamani ya mtu katika kufanya uamuzi kama kiongozi.

Eneo jingine muhimu lililoangaziwa katika warsha hiyo ni elimu ya masuala ya kifedha iliyotolewa na Bw. Howary Kharbush, Mkurugenzi Mshiriki wa Pricewaterhouse Coopers (PwC), ambaye alitoa wasilisho lililopewa anwani isemayo "Uchambuzi wa Taarifa za Kifedha: Mambo ya Msingi kwa Watu Wasio na Taaluma ya Kiuhasibu"

Bw. Kharbush alisisitiza umuhimu wa kuwa na maarifa ya masuala ya kifedha kwa viongozi bila kujali msingi wao wa kitaaluma, ambapo ilisisitizwa kwamba uelewa wa taarifa za kifedha ni maarifa ya msingi anayopaswa kuwa nayo kiongozi katika kufanya uamuzi.

Dkt. Lulu Mahai, Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia UDSM, aligusia umuhimu wa kuzingatia masuala ya kijinsia na kujenga utamaduni shirikishi katika nyanja zote za kiuongozi.

Kwa upande wake Dkt. Innocent Pantaleo, mtaalamu wa HEET-UDSM katika masuala ya Usimamizi na Tathmini ambaye alimwakilisha Naibu Mratibu wa HEET UDSM,Dkt. Liberato Haule, alitoa maelezo ya jumla kuhusiana na Mradi wa HEET ambapo aligusia kuhusu malengo, masuala ya kifedha na maeneo ya msingi yanayoangaziwa katika Mradi ambapo masuala ya jinsia na ushirikishwaji wa makundi mbalimbali ni miongoni mwa maeneo hayo.

Prof. Rose Upor, Rasi, Ndaki ya Insia ambaye alipanda ngazi ya kitaaluma na kuwa Profesa Mshiriki alishukuru kwa fursa na jitihada hizi na kusisitiza umuhimu wake katika kujenga mustakabali bora wa viongozi wanawake UDSM.

Katika warsha hii ilisisitizwa pia kwamba UDSM kitaendelea kuwa kinara katika kujenga mazingira shirikishi ya kitaaluma kwa njia mbalimbali kama ilivyofanywa katika Mradi wa HEET. Aidha, ulisisitizwa umuhimu wa kuwawezesha viongozi wanawake kwa lengo la kuleta mageuzi katika elimu ya juu nchini.

# Mpango Endelevu wa Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa HEET uko Mbioni Kuandaliwa

*Na Ally Mambele, HEET -UDSM*







*Picha za baadhi ya majengo mapya yanayojengwa katika kampasi mbalimbali za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET.*

Katika hatua ya kuhakikisha kwamba Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) unatekelezwa kama ilivyopangwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimeunda timu kwa lengo la kuandaa mpango endelevu wa kusimamia utekelezaji wa Mradi.

Akizungumza na Jarida hili hivi karibuni, Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa HEET- UDSM, alisema kuwa, katika kikao chake cha tatu, kilichofanyika tarehe 26 Oktoba 2023, Kamati Kuu ya Usimamizi wa Mradi ya Chuo iliona kuwa kuna haja ya kuwa na mpango endelevu ili kurahisisha shughuli za Mradi wa HEET, hivyo, kukielekeza Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (PIU) kuandaa mpango huo.

"Ilizingatiwa kwamba kuna mambo mbalimbali ambayo yamechangia kuanzishwa kwa mpango huu. Mambo hayo ni pamoja na nyongeza ya ujenzi wa miundombinu, mapitio ya mitaala, mifumo ya TEHAMA na miundombinu yake, na ujenzi wa kampasi mpya mkoani Kagera na Lindi", amesema Dkt. Haule.

Dkt. Haule ameendelea kueleza kwamba lengo kuu la Timu hii ni kupendekeza mikakati ya kuwezesha Mradi kufanikiwa kwa kiwango cha juu na kupunguza au kuondoa kabisa changamoto zinazoweza kuchelewesha au kukwamisha Mradi kwa kuandaa mpango endelevu wa kusimamia utekelezaji wa Mradi.

Kupitia mpango huu na mbinu mbalimbali, Timu hii iliyoteuliwa pia inakusudiwa kupima ukamilifu wa mradi kwa wakati kwa kuzingatia muda uliowekwa, na hivyo, kuongeza ufanisi kwa ujumla", amesema Dkt. Haule.

Timu hii inajumuisha wataalamu wenye ubobevu na inatarajiwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Mradi unakamilika kwa ufanisi na kuacha athari ya muda mrefu.



*Dkt. Latifa Mbelwa,*
*Amidi wa Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kiongozi wa Timu ya Mpango Endelevu wa Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa HEET UDSM.*

Wajumbe walioteuliwa kuunda Timu hii ni: Dkt. Latifa Mbelwa kutoka Shule Kuu ya Biashara ambaye ni Mwenyekiti wa Timu. Wajumbe wengine ni Dkt. Kwame Ibwe kutoka Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano, Dkt. Paul Ndumbaro kutoka Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, Dkt. Fatma Mohamed kutoka Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia na Bi. Ania Dachi kutoka Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Kwa mujibu wa Dkt. Haule, Timu hii inatarajiwa kuwa na mpango ambao siyo tu kwamba utaharakisha utekelezaji wa Mradi, bali pia utakuwa na manufaa kwa jumuiya nzima ya Chuo. Kwa umoja na weledi wao, Mradi wa HEET- UDSM utakuwa mfano wa kuigwa katika mpango wa usimamizi wa miradi ya elimu ya juu nchini Tanzania.

# Ujumbe wa Naibu Mratibu



## Dkt. Liberato Haule

Naibu Mratibu HEET-UDSM

Tukiwa tunasherehekea Krismasi na mwaka mpya wa 2024, Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kinatoa shukrani za dhati kwa ushirikiano uliotolewa na wadau mbalimbali kuanzia tulipoanza rasmi utekelezaji wa Mradi wa HEET mwezi Juni 2022. Tumepata ushirikiano kutoka kwa wabia wetu mbalimbali.

Serikali imekuwa nasi wakati wote kutusaidia katika utekelezaji wa Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kitengo cha Kitaifa cha Usimamizi wa Mradi (NPIU) wakati wote kimekuwa kikitoa msaada mkubwa wa masuala ya kiutaalamu na kiutaratibu kwa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi UDSM kila kilipoombwa kufanya hivyo. Msaada huo umekuwa ukihusisha masuala ya jumla yanayohusiana na Mradi au masuala mahususi kadiri yanavyoulizwa na wataalamu.

Msaada wa jumla kutoka Kitengo cha Kitaifa cha Usimamizi wa Mradi umedhihirika wazi kupitia mafunzo mbalimbali ya kujenga uwezo yaliyoandaliwa katika ngazi ya wizara. Miongoni mwa mafunzo ya kujenga uwezo ni pamoja na mafunzo kuhusu usimamizi na tathmini, ununuzi, udhibiti wa vihatarishi, usimamizi wa fedha, usalama wa mazingira na kijamii, ushirikiano na viwanda pamoja na masuala ya kijinsia na mahitaji maalum. Ni dhahiri kwamba bila ushirikiano huo madhubuti utendaji wetu katika Mradi usingelikuwa na mafanikio kama ilivyo sasa.

Aidha, Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kinathamini na kutambua ukaguzi wa ndani na nje unaofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kaguzi hizi mbili zinatoa dira kwa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya maadili ya uendeshaji wa mradi. Maoni na mapendekezo yanayotokana na matokeo ya ukaguzi huo yamekuwa na umuhimu mkubwa katika utendaji wa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi.

Vilevile, tunatoa pongezi za dhati kwa timu ya Benki ya Dunia ikiongozwa na Bw. Mathus Kaboko. Wataalamu wetu kutoka Kitengo cha Usimamizi wa Mradi wamepatiwa ushauri, miongozo na uzoefu wa mambo mbalimbali kutoka kwa wataalamu wa Benki ya Dunia kila ilipohitajika. Tangu Juni 2022, kumekuwa na utekelezaji katika maeneo mbalimbali kutoka Benki ya Dunia. Miongoni mwa maeneo hayo ni uendeshaji wa mjadala wa mtu mmojammoja miongoni mwa wataalamu. Mijadala hiyo ni nyongeza ya mijadala ya jumla ambayo pia imehusisha kipindi cha maswali na majibu. Kwa ujumla, msaada uliopatikana kutoka Benki ya Dunia umekuwa ni darasa tosha kwa wataalamu wetu kwani wamepata maarifa mapya na uzoefu katika utendaji wa majukumu yao.

Zaidi ya hayo, mpango wa usaidizi wa utekelezaji wa Mradi umetoa fursa kwa washirika mbalimbali wa utekelezaji wa mradi kubadilishana uzoefu. Mapendekezo kutoka kwa washiriki mbalimbali, Benki ya Dunia na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yamekuwa na umuhimu mkubwa katika utendaji wa wataalamu wa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi.

Kamati ya Kitaasisi ya Usimamizi wa Miradi pia imekuwa ikitoa ushauri, mapendekezo na maelekezo katika vipengele mahususi vya mradi na hivyo, kuwapa shime watendaji kufanya kazi kwa bidii na kwa ufanisi.

Uongozi wa Chuo umekuwa ukifanya kazi kubwa bila kuchoka ili kuhakikisha kwamba Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hili limedhihirika wakati wa usanifu wa miundo mbalimbali, utafiti fuatilizi na mapitio ya mitaala na wakati wa kuandaa miongozo mbalimbali. Uongozi wa Chuo umeendelea kujitolea katika kukisaidia Kitengo na kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba Mradi wa HEET unatekelezwa kwa mafanikio.

Aidha, Kitengo cha Usimamizi wa Mradi kinatoa shukrani za dhati kwa Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa maoni, mapendekezo na wakati mwingine maangalizo kadhaa ambayo wamekuwa wakitoa. Haya yote yamewezekana kwa njia ya ushirikishwaji wa makundi yote ya wadau ambapo wadau hao wamekuwa wakitoa maoni yao kuhusu namna bora ya kufanikisha Mradi.

# Tahariri

## Hatua ya UDSM kuandaa miongozo ya wafanyakazi waambata inastahili pongezi

Katika Jarida hili imeripotiwa kuwa, hivi karibuni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), kimeandaa miongozo mipya ili kuwawezesha wafanyakazi wake kujenga ushirikiano na sekta ya ajira kwa lengo la kuboresha shughuli za ufundishaji na utafiti.

Miongozo iliyotungwa itatumika kama marejeleo muhimu ya kisasa kwa kuongezwa kanuni za msingi, malengo, majukumu, sheria za jumla, na kanuni zinazosimamia wafanyakazi waambata katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, itakuwa ni msaada muhimu kwa jitihada za Chuo Kikuu katika kuimarisha uhusiano kati ya taaluma na soko la ajira kwa kuzingatia uzoefu utakaopatikana na hatimaye kuboresha ufundishaji na kuchochea ubunifu kwa wanafunzi.

Kuandaliwa na hatimaye kupitishwa kwa miongozo hii kunachukuliwa kuwa hatua muhimu katika kukidhi matakwa ya soko la ajira na mahitaji ya sasa ya ulimwengu katika ubadilishanaji wa maarifa na kujenga uhusiano baina ya taaluma na soko la ajira. Suala la wafanyakazi waambata katika vyuo vikuu limekuwa na umuhimu mkubwa kwa miaka mingi sasa ambapo hii imekuwa ni fursa muhimu katika ubadilishanaji wa maarifa baina ya wafanyakazi kupitia taaluma zao mbalimbali na hatimaye kuboresha maarifa yanayotolewa kwa wanafunzi kupitia kwa walimu wao.

Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, wafanyakazi waambata husaidia katika kujenga uhusiano mwema baina ya Chuo na sekta ya ajira pamoja na jamii kwa ujumla, ambapo wafanyakazi hao hubadilishana uzoefu wa kiutendaji. Miongozo hii pia inasaidia kuwafanya wafanyakazi waambata kupata fursa ya kufanya kazi katika sekta ya taaluma na kujiona kuwa ni sehemu muhimu katika ubadilishanaji wa uzoefu katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na utamaduni, utendaji na sera mbalimbali.

Tunazipongeza kwa dhati jitihada za kuandaliwa kwa miongozo hii ambayo inalenga kuwashirikisha wafanyakazi waambata katika jumuiya na utamaduni wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongozo hii ni hatua muhimu katika kujenga uhusiano imara baina ya Chuo na jamii, kuhimiza ujifunzaji kwa vitendo, na kuwajengea wahitimu wetu uwezo kiutendaji kulingana na mahitaji ya jamii pamoja na mabadiliko ya kiulimwengu yanayoendelea.


HEKIMA NI UHURU

HEET — HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

### Uratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

**Mratibu wa Mradi**
Prof. Bernadeta Killian

**Naibu Mratibu wa Mradi**
Dkt. Liberato V. Haule

### Timu ya Uhariri

**Mhariri Mkuu &**
**Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano HEET-UDSM**
Dkt. Dotto Paul Kuhenga

**Wahariri**
Dkt. Lupa Ramadhani (Kiingereza)
Dkt. Mussa Hans (Kiswahili)

**Waandishi:**
Jackson Isdory
Zamda George
Ally Mambele
Mercy Machange
Remmy Wilson

**Mpigapicha:**
Tumaini Kibangala

**Msanifu**
Michael Mwakatobe




# Matukio Katika Picha



Ushirikishwaji Wadau: Mkutano na Viongozi wa UDASA



Prof. John A. M. Mahugija, Mwenyekiti wa UDASA




Ndg. Estelia Mwambene, Mjumbe wa Kamati Tendaji UDASA, CoSS



Dkt. Athuman Mahinda, Mjumbe wa Kamati Tendaji UDASA, CoAF



Dkt. Winfrida Kidima, Mjumbe wa Kamati Tendaji UDASA, CoNAS



## *Warsha ya Udhibiti wa Vihatarishi katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET, Arusha, Disemba 2023*












## *Mahafali ya UDSM Mwaka 2023*










# Mfumo wa Ubunifu wa Usimamizi wa Mradi Kuongeza Ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi

*Na Remmy Wilson, HEET-UDSM*



*Baadhi ya wajumbe wa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakishiriki mafunzo ya Mfumo wa Ubunifu wa Usimamizi wa Mradi yaliyofanyika katika Hoteli ya UDSM Silver Sands, Dar es Salaam, mwezi Novemba, 2023.*

Katika kuelekea kwenye maendeleo makubwa ya teknolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaandaa Mfumo wa kitehama katika Usimamizi wa Miradi. Hayo yameelezwa na Dkt. Kwame Salum Ibwe, Mtaalamu wa Maendeleo ya Dijitali katika Mradi wa HEET-UDSM.

Akizungumza na Jarida hili hivi karibuni, Dkt. Ibwe alitoa ufafanuzi kuhusu hatua ya kuridhisha ya maendeleo ya mfumo huu huku akiushukuru Mradi wa HEET kwa ufadhili wa Mradi huu.

Mfumo huu jumuishi ulioandaaliwa kwa ustadi wa hali ya juu na Dkt. Ibwe pamoja na wataalamu wenzake, umehusisha vipengele muhimu vitakavyosaidia kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa Mradi.

Miongoni mwa maeneo muhimu katika mfumo huu, kama yalivyoangaziwa na Dkt. Ibwe, ni usimamizi wa mradi wenyewe, ambapo mfumo huo unazingatia usimamizi jumuishi katika kazi inayofanyika, tarehe ya makataa na kuhakikisha kwamba wanamradi wote wanawajibika ipasavyo. Mfumo huu utazipa mamlaka za usimamizi fursa ya kusimamia Mradi moja kwa moja, kuimarisha ushirikiano na mawasiliano baina wa washiriki wa Mradi.

Kuhusiana na utekelezaji wa Mradi wa HEET, Dkt. Ibwe pia alisema mfumo huo utahusisha maeneo mbalimbali ambayo ni usimamizi wa kazi, usimamizi wa fedha; usimamizi wa waendeshaji wa Mradi na kalenda ya matukio; ambapo utawawezesha wadau mbalimbali kufuatilia majukumu mbalimbali na makataa ya utekelezaji wake. Sifa hizi za mfumo zitawezesha kuweka mpango na uratibu, kupunguza kuchelewa kukamilika kwa mradi na hivyo kuongeza ufanisi.

“Kipengele kingine cha kipekee cha mfumo huu ni uwezo wake wa kufuatilia na kusimamia maendeleo ya wanafunzi wanaofadhiliwa na Mradi wa HEET. Hali hii inahakikisha kwamba mipango ya elimu inawezeshwa ipasavyo huku ikiwiana na malengo ya Taasisi na hivyo kuwezesha usimamizi wa Maendeleo kwa wanafunzi wanaofadhiliwa na Mradi wa HEET”, amesema Dkt. Ibwe.

Dkt. Ibwe pia alieleza kujumuishwa kwa uwezo thabiti wa kuripoti katika mfumo ambapo watumiaji wanaweza kutoa ripoti za kina za mradi, ikiwa ni pamoja na maelezo ya maendeleo ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali, matumizi ya fedha na mambo mengine muhimu. Ripoti hizohizo zitasaidia sana katika kufanya uamuzi sahihi na kuwezesha mawasiliano ya uwazi na wadau.

Pia, alionesha matumaini yake katika athari za mabadiliko ya Mfumo wa Usimamizi wa Mradi, kwa kusema, “Mfumo unadhihirisha hatua kubwa na muhimu iliyofikiwa katika ufanisi kwenye usimamizi wa Mradi na matumizi ya dijitali. Hali hii inaendana na dhamira ya HEET UDSM ya kukuza ubora katika elimu na utafiti kwa kutoa jukwaa la kisasa katika jitihada za mipango yetu ya kitaaluma na kiutawala”.

Kadiri mfumo unavyoendelea, jumuiya ya Chuo kupitia Mradi wa HEET-UDSM inasubiria kwa hamu na ghamu kukamilika kwa mfumo huu, ambao utainua kiwango cha utekelezaji wa Mradi na uangalizi wake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

# UDSM Waandaa Mwongozo wa Uambatishaji wa Wafanyakazi

*Na Mercy Machange, HEET-UDSM*




*Dkt. Kennedy Hosea, Mratibu wa Mradi wa HEET Kitaifa (katikati, waliokaa), Prof. Bonaventure Rutinwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma (kushoto, waliokaa) na Mratibu wa Mradi wa HEET katika eneo la uhusiano wa taaluma na tasnia ya ajira, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (kulia, waliokaa) wakiwa na baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati wa kikao cha kujadili ushirikiano wa taaluma na tasnia ya ajira kilichofanyika UDSM hivi karibuni.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Mradi wa HEET kimechukua hatua mbalimbali katika kuendana na mahitaji ya soko la ajira kwa kuandaa mwongozo utakaowezesha wanataaluma kuambatishwa katika tasnia mbalimbali ili kuboresha shughuli za utafiti na ufundishaji.

Akizungumza na Jarida hili, Profesa Neema Mori, Mkurugenzi wa Huduma kwa Umma, alieleza kwamba mwongozo huu utakuwa ni rejeleo muhimu katika kubaini malengo, wajibu, sheria na kanuni zitakazoongoza mchakato wa uambatishaji wa wanataaluma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

“Tunalenga kuwapatia wahitimu wetu maarifa yanayojikita katika nadharia na stadi zinazohitajika katika maeneo yao ya ubobezi. Jitihada hizi zinaonesha dhamira yetu ya dhati katika kuzalisha wahitimu watakaokuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto watakazokutana nazo katika matumizi ya maarifa waliyojifunza watakapokuwa wanatekeleza majukumu yao”, amesema Prof. Mori.

Aliongeza kuwa, miongozo hii ni ishara ya mafanikio na msaada muhimu kwa mpango wa Chuo Kikuu katika kuimarisha uhusiano kati ya taaluma na tasnia ya ajira ambapo uzoefu wa ufanyaji kazi kwa vitendo utasaidia kukuza ubora katika ufundishaji na kuchochea ubunifu wa wanafunzi.

Wakati huhuo Dkt. Fatuma Simba, Mtaalamu wa HEET-UDSM kwa upande wa ushirikishwaji wa sekta, binafsi, alieleza umuhimu wa wafanyakazi waambata katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kusisitiza kwamba mwongozo unaweka msingi na kubainisha vipengele mbalimbali vinavyohusiana na upatikanaji na usimamizi wa wafanyakazi waambata katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

“Chuo kinatambua umuhimu wa kuboresha programu za kitaaluma na kwamba wafanyakazi waambata wana nafasi kubwa katika kufanikisha dhima hii muhimu. Wafanyakazi wa aina hii wamekuwa na manufaa makubwa katika huduma wanazotoa katika vyuo mbalimbali ulimwenguni. Kwa hiyo, mwongozo huu umeandaliwa ili kuhakikisha kwamba ushirikiano huu unafanyika kwa ufanisi”, amesema Dkt. Simba.

Dkt. Simba amesisitiza kwamba, ushirikiano huu, zaidi ya kuhakikisha kwamba UDSM kinaendelea kutoa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya jamii, utakipatia Chuo athari chanya za kijamii na kiuchumi.

Wakati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikiendelea kupiga hatua ya maendeleo, mwongozo huu utakuwa ni hatua muhimu ya kimkakati katika kukuza ushirikiano baina ya Chuo na tasnia mbalimbali, kuimarisha ufundishaji kwa vitendo, na kuwawezesha wahitimu kukabiliana na mazingira ya kitaalamu yanayobadilika mara kwa mara.



*Dkt. Hadija Kweka, Mratibu wa Mradi wa HEET katika eneo la uhusiano wa Taaluma na tasnia ya ajira, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.*



*Prof. Goodluck Urassa, Shule Kuu ya Biashara, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*



*Dkt. Kennedy Hosea, Mratibu wa Mradi wa HEET Taifa.*



*Bonaventure Rutinwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, UDSM.*

# Taasisi za Elimu ya Juu zatakiwa kuimarisha Mkakati wa Udhibiti wa Vihatarishi katika Mradi wa HEET

Na Dotto Kuhenga, HEET-UDSM



*Dkt. Kennedy Hosea, Mratibu wa Mradi wa HEET Taifa akizungumza na washiriki wa Warsha ya Udhibiti wa Vihatarishi katika utekelezaji wa Mradi wa HEET iliyofanyika Jijini Arusha hivi karibuni.*

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe amezitaka Taasisi za Elimu ya Juu kuzingatia suala la udhibiti wa vitaharishi katika utekelezaji wa Mradi wa HEET ili kuleta mafanikio yanayotarajiwa.

Prof. Mdoe aliyasema hayo katika mafunzo ya maafisa wanaohusika kwa namna moja ama nyingine na Usimamizi wa Mradi wa HEET kutoka taasisi mbalimbali. Mafunzo hayo yalifanyika katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia – Nelson Mandela, Arusha.

"Ni muhimu Taasisi zinazotekeleza Mradi huu kuhakikisha kwamba zinazingatia suala la udhibiti wa vihatarishi ambavyo vinaweza kukwamisha kufikiwa kwa malengo na kuzingatia muda uliopangwa", amesema Prof. Mdoe.

Prof. Mdoe alisisitiza kuwa: "Tunakaribia muda wa kufanya tathmini ya kati ya Mradi ambayo inatarajiwa kufanyika Mei, 2024 ambapo kila taasisi inapaswa kufikia malengo kwa kati ya 40% na 50% ya utekelezaji wa Mradi katika kipindi hiki. Hivyo, ni muhimu kuwa na uelewa kuhusu vihatarishi ambavyo vinaweza kuwa kikwazo katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi na kuona namna ya kudhibiti vihatarishi".

Naibu Katibu Mkuu alizihadharisha Taasisi hizi kwamba bado ziko katika 12% ya maendeleo ya Mradi na kuwataka kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kwamba wanafikia malengo yanayotarajiwa.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, na kufanyika kwa siku tano kuanzia tarehe 4 hadi 8 Disemba, 2023, yalishirikisha washiriki zaidi ya 140. Mafunzo yalihusisha mada sita ambazo ni: mfumo wa udhibiti wa vihatarishi, usajili wa vihatarishi, mpango wa utekelezaji wa udhibiti wa vihatarishi, mpango wa kupunguza vihatarishi, na utoaji wa ripoti kuhusu vihatarishi.

Wakati huohuo, Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa HEET, Dkt. Kennedy Hosea amesisitiza umuhimu wa kutoa mafunzo kwa washiriki wa mradi kwa kuzingatia kwamba Mradi unaweza kukabiliwa na vitaharishi vya hali ya juu kutokana na vikwazo vya kimaadili, kimazingira, kijamii, kitaasisi na uwezo katika utekelezaji na uendelevu wa Mradi. "Kwa hiyo, kila Taasisi inayohusika na utekelezaji wa Mradi itapaswa kuzingatia namna bora ya kudhibiti vitaharishi hivi" Amesema Dkt. Hosea.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maafisa 13 walishiriki mafunzo haya. Maafisa hawa ni Dkt. Liberato Haule (Naibu Mratibu wa Mradi), Janneth Mwamwenda (Meneja Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi), CPA Ally Mringo (Mtaalam wa Usimamizi wa Fedha), Dkt. Paul Ndumbaro (Mtaalamu wa Maendeleo ya Miundombinu); na Prof. Pendo Malangwa (Mkurugenzi, Kitengo cha Udhibiti Ubora na mwakilishi wa Mratibu wa Mapitio ya Mitaala).

Wengine ni Dkt. Fatuma Simba (Mtaalam wa Ushirikishwaji wa Sekta, Binafsi), Dkt. Dotto Kuhenga (Mtaalamu wa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma); Paul Riziki (Afisa Ununuzi na Mwakilishi wa Mtaalamu wa Ununuzi); Dkt. Kwame Ibwe (Mtaalam wa Maendeleo Teknolojia katika Elimu na Miundombinu ya Dijitali), Dkt. Omar Zuber (Mratibu wa Udhibiti wa Vihatarishi); Ania Dachi (Kaimu Mtaalamu wa Masuala ya Usimamizi na Tathmini); Hadija Mtani (Mwakilishi wa Mtaalam wa Masuala ya Jinsia na Watu wenye Mahitaji Maalum); Petro Mselewa (Afisa Mwandamizi wa Sheria) na Otilia Rutashobya (Mashuri wa Masuala ya Sheria).

# Shairi




## "Nyota *yang'ara* Mlimani"

**Na Rajabu Makacha**

Kwenye kilima kitukufu, uchomozapo moto wa hekima,
Ahadi ya HEET, hadithi isimuliwayo,
Safari imeanzishwa, ya masafa ya kiuchumi,
Wanafunzi lufufu kukusanyika, matumini yamejaa mioyoni,

Mitaala yarindima, kwa sauti zenye uhalisi,
Kisemwacho ni viwanda, kwa matarajio yajayo,
Stadi za ulimwengu halisi, ndio nyenzo kibindoni,
Kwenye chombo cha elimu, vimesimama vipo madhubuti.

Ajira, kuwa nyota ya jaha, kuitwaa inatia raha
Ndoto za mtandao wa Ulimwengu, ni amali zilotukuka,
Imejenga miunganiko, daraja kuifikia kesho,
Kwenye shangwe la maendeleo, kulifuata kwa madaha.

Imebeba ubunifu, kwa busu la teknolojia,
Mafanikio  kuongezeka, kuziba ufa wa taaluma,
Yasemwayo ni usasa, wimbo uimbwao darasani,
Mahali pakuzwapo akili, kuwa pevu na imara.

Ndoto na sarafu za dhahabu, za uzito wa thamani,
Zavumisha nguvu ya fedha, zielekeazo kwenye dira,
Mkono usaidiao kiungwana, kwa neema za ufadhili,
Kwenye mawindo ya hazina, nafasi ya ujifunzaji.

Maono ya kimataifa, ya upeo kimandhari,
Ya mbawa ziliotandaa, na nyingi mpya shauku
Zisemwazo kimataifa, kubadilishana uwezo,
Kwenye kitovu cha maarifa, rangi zaungana.

Kamba za maadili, mesokotwa kwa makini,
Maadili ya jamii, yasiyomithilika,
Dhamana edelevu, za udhati wa mioyoni,
Kwenye kitovu cha elimu, tamko limetimia.

Mchezo wa mipango, mwelekeo tofauti,
Mabadiliko ya programu, penye kiza pamekuwa mwanga
Mchanganyiko wa machaguo, hili linasisimua,
Safari ya mwanafunzi, kwenye mambo malimbali.

Hakika malengo ya HEET, yana  mshindo mkubwa,
Akili na ndoto viliunganishwa, bega kwa bega,
Sikiliza kwa karibu, usikie matamu yasemwayo,
Wimbo wa wanafunzi, mageuzi ya kishindo.

Upepo wa wasomi, unavuna kutoka mlimani,
Unaunda mafanikio, ya kukuza maarifa,
Sikiliza kwa makini, usikie mazuri yajayo,
Mboni ya UDSM 2061, Hekima ni Uhuru.



# Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar Yatembelea UDSM-HEET

Na Tumaini Kibangala, UDSM-HEET




*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na wajumbe wa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati Kamati ya Kudumu hiyo ilipotembelea UDSM kujifunza kuhusu utekelezaji wa Mradi wa HEET.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma akisaini Kitabu cha Wageni katika Ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye (hayupo pichani) wakati Kamati hiyo ilipotembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kujifunza kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa HEET.*




*Dkt. Liberato Haule,*
*Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET,*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi wamefanya ziara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tarehe 16 Novemba, 2023 kujifunza mambo mbalimbali kuhusiana na utekelezaji wa Mradi wa HEET.

Kamati hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Makamu Mwenyekiti Mhe. Dkt. Sudi Nahoda Hassan ilikipongeza Chuo kwa hatua kubwa iliyopiga katika utekelezaji wa Mradi wa HEET wakibainisha kwamba mengi waliyoyasikia na kuyashuhudia yatazingatiwa kwa manufaa ya Taasisi wanayotoka.

Wajumbe wa Kamati pia walioongozana na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Prof. Mohammed Makame ambapo chuo anachokiongoza ni miongoni mwa wanufaika wa Mradi wa HEET.

Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye alisema kwamba Chuo kimefarijika kutembelewa na ugeni huu ambapo pia alitumia wasaa huo kueleza kwa ufupi historia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maendeleo yaliyofikiwa na hatua ambazo Chuo kinachukua kuhakikisha kwamba Mradi wa HEET unafanikiwa

Dkt. Liberato V. Haule, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM akiwa na wajumbe wa Kitengo cha Usimamizi wa Mradi alifafanua kwa kina kuhusu hatua ambazo Chuo kimefikia katika utekelezaji wa Mradi na kubainisha maeneo ya ushirikiano baina ya UDSM na SUZA ili kuwa na matoleo bora katika masuala ya kitaaluma na maeneo mengine muhimu.

Wajumbe hao walitoa shukurani zao za dhati kwa UDSM ambapo pia walionesha kuthamini dhamira na juhudi za hali ya juu zinazochukuliwa na UDSM kuhakikisha kwamba kinafikia malengo ya Mradi. Dhamira na jitihada hizi zilichukuliwa kama funzo kwa SUZA na Kamati kwa ujumla.

HEKIMA NI UHURU

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

## Mawasiliano


Naibu Mratibu: +255 765 939 958

Mhariri Mkuu: +255 755 172 570

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
Jengo la Cranford Pratt,
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani
Barabara ya Chuo Kikuu, 16103 Ubungo
S.L.P. 35091
Dar es Salaam, Tanzania

heet@udsm.ac.tz Heet Udsm www.udsm.ac.tz